TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION (TARO)

# Mapendekezo ya marekebisho ya Rasimu ya Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa (2021)



SANAA RIGHTS PROGRAM






Imefadhiliwa na: Norwegian Embassy Dar es Salaam

## SEKTA YA SANAA NA UTAMADUNI TANZANIA

Mapendekezo haya yameandaliwa kwa kuzingatia weledi wa tasnia ya sheria katika uandishi wa miswada, sheria zinazolinda haki za binadamu nchini, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) , mikataba ya kimataifa inayolinda haki za kitamaduni na haki nyingine za binadamu, uzoefu wa taaasisi katika kushiriki kwenye shughuli za sanaa na maoni ya wasanii kwenye mikutano mbalimbali tuliyoratibu.

**Utangulizi:**
Tanzania Artists Rights Organization **(TARO)** ni asasi ya kiraia inayojishughulisha na utetezi wa haki na maslahi ya wasanii nchini. Pia **TARO** inafanyakazi kama watetezi wa haki za kitamaduni, inachangia maendeleo ya sekta ya Sanaa na Utamaduni kwa njia ya uhamasishaji wa uhuru wa kutoa maoni kupitia kazi za Sanaa, ulinzi wa haki na maslahi ya wasanii, kutetea usawa wa kijinsia kwenye sekta na kuhamasisha weledi wa kitaaluma kwenye shughuli za Sanaa.

Mapendekezo yameandaliwa na TARO kwa kuzingatia weledi wa tasnia ya sheria katika uandishi wa miswada, sheria zinazolinda haki za binadamu nchini, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977), mikataba ya kimataifa inayolinda haki za kitamaduni na haki nyingine za binadamu, uzoefu wa taaasisi katika kushiriki kwenye shughuli za sanaa na maoni ya wasanii kwenye mikutano mbalimbali.

Mapendekezo haya ni sehemu ya shughuli ya mradi wa SANAA RIGHTS, unaofadhiliwa na Ubalozi wa Norway-Dar es salaam. Mradi huu unatekelezwa na TARO kwa ushirikiano na Culture Development East Africa (CDEA).

**Dhumuni:**

Dhumuni la mapendekezo haya ni kama ilivyoorodheshwa hapo chini: -

i. Kuwalinda wasanii ili kufurahia haki zao za kibinadamu katika utekelezaji wa shughuli za Sanaa na utamaduni.

ii. Kuisaidia serikali katika kuboresha mazingira rafiki ya kibiashara kwenye sekta ya Sanaa na utamduni

iii. Kuboresha sheria zinazoongoza sekta ya Sanaa na utamaduni kwa kuhamasisha ushiriki na ushirikishwaji wa wadau katika utungaji wa sheria.

MAWASILIANO
SIMU: +255785769223
BARUA PEPE: tarotanzania@gmail.com

TARO
TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION

CDEA
CULTURE AND DEVELOPMENT EAST AFRICA

Funded by:
Norwegian Embassy
Dar es Salaam

**Dondoo muhimu za mapendekezo:**

Mapendekezo haya yamejikita katika kuzungumzia masuala mbalimbali yanayoweza kuathiri sekta ya Sanaa na utamaduni kupitia kanuni pendekezwa kama yalivyoelezewa kwa ufupi hapo chini: -

| | | |
|---|---|---|
| i | Utunzi wa kanuni zinazoongoza sekta ya Sanaa na utamaduni ambao hauzingatii na unavunja haki za binadamu na kukinzana na katiba ya nchi. | • Kuminya uhuru wa maoni kwenye kazi za Sanaa.<br>• Kuvunja haki ya kufanya kazi<br>• Kuvunja haki ya kusafiri<br>• Kuvunja haki ya kufurahia utamaduni.<br>• Kupuuzia masuala ya kijinsia |
| ii | Utunzi wa kanuni pendekezwa unaobadilisha malengo ya uundwaji wa baraza la Sanaa la Taifa | • Baraza kudhibiti shughuli za Sanaa badala ya kulea ukuaji wa Sanaa<br>• Baraza kuharibu kazi za Sanaa<br>• Kanuni pendekezwa kuingilia uhuru wa asasi za kiraia<br>• Baraza kujishughulisha na utatuzi wa migogoro |
| iii | Baraza kuingilia utendaji wa mamlaka zingine za serikali | • Uhamiaji<br>• Mamlaka ya mawasiliano (TCRA)<br>• Polisi<br>• Mahakama<br>• Ofisi ya Takwimu ya Taifa |
| iv | Kanuni pendekezwa kutozingatia na kuheshimu mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu | • International Convenant of Economic, Social and Cultural Rights (ICESCR) 1966<br>• Universal Declarations of Human Rights (UDHR)1948 |

# YALIYOMO


i. Mwaka wa rasimu, Lebo ya Sanaa, Sheria iliyotumika……………….…...………….……..4

ii. Maombi Kutoa elimu kwa Wasanii ni kinyume cha Katiba ya Nchi…………….……..…….5

iii. Baraza kuratibu kazi za Sanaa ni kupingana na soko huria……………………………….….5

iv. Kibali kufanya Sanaa nje ya Nchi ni kinyume na Haki za Binadamu…………....…….…….5

v. Kibali kwa Msanii kwenda kufanya Sanaa nje ya Nchi ni kupitwa na wakati……...……….6

vi. Kusajili wadau wa Sanaa ni tishio kukandamiza Haki za kikatiba………...…………...…….7

vii. Kuzuia kusajiliwa kwa Chama cha Sanaa chenye malengo sawa na chama kilichokwisha sajiliwa…………………...……………………………………………..……………….…….8

viii. Mashirikisho yanapaswa kuzingatia misingi ya demokrasia………………………......…..9

ix. Kuharibu kazi za Sanaa zinazokinzana na Sheria kuzingatie haki…………….……..…..10

x. Kumfutia msanii usajili wa Baraza ni kumvunjia haki zake za Binadamu………...…...…...10

xi. Kuweka kibali ili Msanii aweze kufanya kazi ya Sanaa……….…………………………....11

xii. Maafisa wa Baraza kupewa mamlaka yaliyopitiliza kuliko Polisi……...…...…………….....12

xiii. Baraza kuingilia uhuru wa Asasi za kiraia……...…………...……………….……….......13

xiv. Vibali kwa Wasanii, wadau wa Sanaa au Vikundi vya Sanaa kwenda nje ya Nchi ……......14

xv. Vibali vya kuingia Nchini kufanya Sanaa ni urasimu…………….…………..………..…15

xvi. Uthibitisho wa uwezo wa kumudu gharama kwa muandaaji wa kigeni……………….…....16

xvii. Uandaaji wa Matukio na masuala ya Kimaadili…………………………………………….17

xviii. Kazi za Sanaa katika vyombo vya Habari siyo jukumu la Baraza………………..…………18

xix. Baraza halipaswi kujishughulisha na utatuzi wa migogoro…………………..………..........18

xx. Uandaaji wa kanuni pendekezwa haijazingatia usawa wa kijinsia ………...……………….19

xxi. Hitimisho…………………………..………………………………………..………......20

a) **Mwaka wa Rasimu**.
Rejea kifungu cha **1** cha rasimu ya kanuni pendekezwa, kinaonyesha rasimu imeumdwa mwaka 2021.

**Mapendekezo:**
Rasimu itambulike kwa mwaka uliyoipitisha kuwa sheria, mfano 2023.

**b) Lebo ya Sanaa kuwa Asasi ni kuondoa thamani ya kibiashara kwenye sanaaa**

Kifungu cha **3** cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinatambua kuwa **lebo ya Sanaa** ni asasi. Hii inaziondolea lebo za Sanaa sifa ya kufanya biashara**.** Usajili ukizitambua kuwa ni asasi zitashindwa kuingia kwenye ushirika wa kibiashara na taasisi kubwa za kibiashara ndani na nje ya nchi kwa malengo ya kibiashara. Ambapo, Lebo za Sanaa zitapoteza sifa ya kuwa taasisi za kibiashara.

**Mapendekezo:** Lebo za Sanaa zinapaswa kutambuliwa kama taasisi zilizoundwa kufanya kazi za Sanaa kwa malengo ya kugeuza kazi za Sanaa kuwa biashara. Kusajili lebo za Sanaa kuwa asasi ni kuondoa thamani ya kibiashara kwenye kazi za Sanaa. Sanaa itaendelea kuonekana sio ajira, sio biashara lakini ni jambo la kujitolea.

**c) Sheria iliyotumika kwenye kanuni imefutwa miaka 39 iliyopita**

Rejea kifungu cha **3** cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinachotafsiri neno **"sheria",** kimeitaja sheria iliyofutwa na kuondolewa kwenye matumizi ambayo ni **Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa.**

**Mapendekezo:** Marekebisho ya sheria, namba 5 ya 2019 yalifanya makosa makubwa kwa kurekebisha **Sheria ya Sanaa ya 1984** kwa kutumia jina la **Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa ya Mwaka 1974** ambayo imefutwa tangu 1984 kupitia **Sheria ya Sanaa, namba 23 ya 1984**. Ili makosa yasiendelee kuwepo rasimu ya Kanuni pendekezwa inapaswa kuacha kutumia maneno **"Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa"** au kwa kiingereza **National arts Council act.** Bali inapaswa kutumia jina sahihi la sheria ambalo **ni Sheria ya Sanaa ya Taifa, namba 23 ya 1984.**

Mnamo mwaka 1984 Baraza la Sanaa la Taifa liliunganishwa na Baraza la Muziki la taifa kwa kutungwa sheria mpya iitwayo **Sheria ya Sanaa ya Taifa, namba 23 ya 1984**, ambayo ilifuta **Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa ya mwaka 1974** na **Sheria ya Baraza la Muziki la Taifa ya mwaka 1974**. Hivyo basi kwa maelezo hayo mafupi **Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa** kimsingi haipo na siyo sahihi kuendelea kuitaja

a) **Kufanya maombi kwa kamati za Sanaa za wilaya au mkoa au BARAZA ili kutoa elimu kwa wasanii ni kinyume na katiba ya nchi**.

Kifungu cha **5,** kifungu kidogo cha **(2)** na **(3)** cha rasimu ya kanuni pendekezwa**,** inavitaka vyama, mashirikisho au mtandao unaojihusisha na kazi za sanaa kufanya maombi kwenye kamati za Sanaa za wilaya au mkoa au BARAZA zinapotaka kutoa mafunzo kwa wasanii. Kanuni hii inakinzana na katiba ya nchi kwa kuweka masharti ya mtoaji elimu kwa wasanii lazima afanye maombi ya kutoa elimu ili wasanii waweze kufurahia haki yao ya kikatiba ya kupewa taarifa muhimu zinazohusiana na Maisha yao. Ieleweke kuwa maombi yanaweza kukubaliwa au kukataliwa.

Rejea ibara ya **18,** ibara ndogo **(2)** ya **katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)** kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara (Toleo la Kiswahili la mwaka 2000) inaelekeza: -

*"Kila raia anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali nchini na duniani kote ambayo ni muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi, na pia juu ya masuala muhimu kwa jamii."*

**Mapendekezo:** Kifungu hicho kinapaswa kufutwa kwani kinavunja haki za binadamu zinazolindwa na katiba ya nchi na mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia. Kinatengeneza mazingira ya siku zijazo kuzuia wasanii kupewa taarifa zao muhimu kuhusiana na kazi zao za Sanaa. Pale watakapotaka kupewa mafunzo ya haki zao itakua lazima mtoaji mafunzo aombe ambapo anaweza kukubaliwa au kukatiwa kitu ambacho ni kinyume na haki za binadamu na katiba ya nchi.

TARO
TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION

**b) Kulazimisha maonesho, matamasha, tuzo au mashindano kuratibiwa chini ya BARAZA ni kupingana na misingi ya soko huria na uhuru wa kufanya kazi za sanaa.**

Kifungu cha **7**, kifungu kidogo cha **3** cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinaelekeza kuwa shughuli (matukio) ya maonyesho, matamasha, tuzo au mashindano kwenye shughuli za sanaa kuratibiwa chini ya BARAZA. Ambapo muandaaji ataomba kibali na kama atapewa haitaishia hapo, BARAZA wataendelea kuingilia uratibu wa tukio lake. Tanzania ni nchi mwanachama na imesaini mkataba wa kimataifa wa kulinda na kuheshimu haki za binadamu (haki za kitamaduni) tangu **1976**. Ibara ya **(15)**, ibara ndogo ya **(3)** ya **Mkataba wa kimataifa wa haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni (1966)** inaelekeza kuwa *nchi mwanachama zimejidhatiti kuheshimu* ***uhuru muhimu*** *kwa utafiti wa kisayansi na shughuli za ubunifu*. Kifungu hicho cha rasimu ya kanuni kinavunja mkataba huu wa kimataifa kwa kudhoofisha uhuru muhimu wa shughuli za kibunifu. Sanaa ni miongoni mwa shughuli za kibunifu.

Ikumbukwe kuwa matukio hayo ni biashara ndani ya soko huria lenye ushindani. Tanzania tumeingia mkataba wa kimataifa wa masoko huria na pia tunasheria za kulinda masoko huria, kanuni hii inavunja na kutokuheshimu mkataba huo wa kimataifa na sheria za ndani za ushindani wa kibiashara. Pia kanuni hii inaingilia uhuru katika ufanyaji wa kazi za Sanaa na itapelekea baadhi ya wasanii, wadau na wawekezaji kwenye sanaa kushindwa kufanya kazi za Sanaa kwa umahiri. Kanuni hii inatengeneza mazingira ya BARAZA kuwaelekeza wasanii, wadau na wawekezaji namna ya kufanya biashara ya Sanaa kitu ambacho hakiendani na biashara ya Sanaa.

Shughuli za kibiashara zinahusisha siri za ushindani wa kibiashara, kama BARAZA watajiingiza kuratibu shughuli za wafanyabiashara mbalimbali kwenye ushindani wa biashara ya sanaa, itafikia hatua wafanyabiashara watapoteza imani na BARAZA wataacha kuwekeza kwenye Sanaa. Wataona siri zao za ushindani wa kibiashara zinavuja.

**Mapendekezo:** Kifungu hicho kibadilishwe na BARAZA wasihusike kuratibu shughuli yoyote inayoendeshwa binafsi labda kwa maombi ya mwenye shughuli. BARAZA iweke viwango vya utekelezwaji wa matukio ya Sanaa nchini kwa kuzingatia haki za binadamu, utawala bora, sheria za ndani na za kimataifa.

c) **Kuomba kibali kwa msanii kwenda kufanya shughuli za Sanaa nje ya nchi inavunja haki za msingi za binadamu za kufanya kazi na uhuru wa shughuli za kibunifu.**

Kifungu cha **31** cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinaelekeza kuwa msanii anapaswa kupata kibali cha baraza ili kwenda nje ya nchi kufanya kazi za Sanaa.

Haki ya kufanya kazi ni haki ya binadamu inayolindwa na katiba ya nchi na sheria za kimataifa. Haki ya kusafiri kwenda nje ya nchi pia ni haki ya binadamu inayolindwa na katiba ya nchi. Kila mwananchi ana haki ya kufanya kazi sio lazima apewe ruhusa na mamlaka ndio afanye kazi. Kuomba kibali cha kwenda nje ya nchi kufanya kazi ya kawaida kabisa ya sanaa ni kuvunja katiba ya nchi kwa kumwekea mwananchi masharti ya kumruhusu au kumkatalia kufurahia haki yake ya binadamu aliyohakikishiwa kuifurahia na katiba ya nchi.

Rejea ibara ya **22,** ibara ndogo **(1)** ya **katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)** kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara (Toleo la Kiswahili la mwaka 2000) inaelekeza: - *"Kila mtu anayo haki ya kufanya kazi"*

**Mapendekezo:** Kanuni hiyo ibadilishwe ili kuondoa neno kibali na kuweka neno kutaarifu **(Notification).** Taarifa itolewe kabla ya kuondoka ua siku kadhaa baada ya msanii kurudi nchini. Taarifa hiyo isiwe kigezo cha kumzuia msanii kusafiri nje ya nchi kwenda kufanya kazi zake za sanaa, kwasababu msanii ana haki ya kwenda kuishi atakako, anahaki ya kuingia na kutoka nje ya nchi kwa mujibu wa ibara **17,** ibara ndogo ya **(1)** ya katiba tajwa hapo juu

**Kumkataza msanii asiende nje ya nchi kufanya kazi ya Sanaa kwasababu ya kibali kumepitwa na wakati, hakuendani na mazingira ya biasahara ya sanaa na kuna kandamiza uhuru wa msanii kufanya kazi za Sanaa.**

Kanuni ya **9,** kanuni ndogo ya **(3)** ya rasimu ya kanuni pendekezwa, inaelekeza kuwa hakuna msanii kwenda nje ya nchi kushiriki mashindano ya kuiwakilisha nchi mpaka apate kibali. Kanuni hii inarudisha nyuma maendeleo ya Sanaa na utamaduni kwa kuweka urasimu, ugumu na udhibiti usio na tija kwa wasanii kushiriki katika shughuli za Sanaa za kimataifa. Pia imejikita katika kuwadhibiti wasanii kuliko kuwasaidia. Haina faida yoyote kwa taifa wala sekta. Inaimarisha ukandamizaji wa uhuru wa kufanya kazi za Sanaa (shughuli za kibunifu). Kanuni hii inalazimisha wasanii kuwaogopa baraza kwa kuhofia kunyimwa vibali katika shughuli zao za biashara ya Sanaa na masuala ya kitamaduni.

Ibara ya **(15)**, ibara ndogo ya **(3)** ya **Mkataba wa kimataifa wa haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni (1966)** inaelekeza kuwa *nchi mwanachama imejidhatiti kuheshimu* ***uhuru muhimu*** *kwa utafiti wa kisayansi na shughuli za ubunifu*. Kifungu hicho cha rasimu ya kanuni kinavunja mkataba huu wa kimataifa kwa kudhoofisha uhuru muhimu wa shughuli za kibunifu.

Kanuni imejikita nje ya lengo kuu la uundwaji wa baraza ambalo ni kusiadia ukuwaji wa sekta ya Sanaa na utamaduni na siyo kudhibiti sekta. Tayari sheria za kudhibiti sekta zipo nyingi sana. Mfano: Sheria za mamlaka ya mawasiliano, uhamiaji, sheria za kimataifa za diplomasia na makosa ya jinai zinaongelea masuala yote ya raia wa nchi moja awapo nchi nyingine.

**Tafakuri**: Vipi msanii akienda bila kibali akashinda mashindano hayo akaipa nchi heshima kimataifa, akirudi atapewa adhabu? Vipi msanii yuko nje akapata hiyo fursa asubiri BARAZA wampe kibali ndio ashiriki? Kuna gharama kubwa wasanii wanatumia kutafuta fursa za nje, vipi akatumia gharama zake akapata fursa alafu akamnyimwa kibali, baraza litamfidia gharama zake? Kanuni hii imebeba hasara nyingi kuliko faida kwenye sekta.

**Mapendekezo:** Kanuni hiyo tajwa inapaswa kurekebishwa na kumtaka msanii kutoa taarifa au kuomba atambuliwe na BARAZA kabla ya kushiriki tukio au mara baada ya kushiriki tukio. Msanii asitakiwe kuwa na kibali cha aina yoyote kushiriki fursa za kimataifa. Kibali hiki kinatoa nguvu ya ziada na mwanya kwa maafisa wa baraza kumkandamiza msanii.

## Kusajili wadau wa Sanaa ni tishio la kukandamiza haki za kikatiba za uhuru wa kutoa maoni, haki za kitamaduni na uhuru wa kushiriki katika shughuli za umma hususani Sanaa.

Kanuni ya **12** na **13** ya rasimu ya kanuni pendekezwa inaelekeza lazima kila mdau wa Sanaa nchini asajiliwe na BARAZA. Hiki kifungu hakina, weledi, mantiki, uhalisia pia kinavunja haki za binadamu. Kifungu hiki kinakinzana na malengo makuu ya uundwaji wa baraza ambayo ni kulinda na kukuza tamaduni za kitanzania.

Tamaduni zinawezaje kulindwa na kukua endapo kuziishi lazima ufuate urasmi na uzilipie kila mwaka kupitia usajili. Ikumbukwe kushiriki kwenye shughuli za Sanaa ni haki ya binadamu ya kufurahia utamaduni.

Inamaanisha mashabiki wote wa Sanaa zote wasajiliwe na BARAZA ndio wajishughulishe na sanaa. Inamaanisha wanasheria wasifanye kazi zao za kisheria kuwashauri wasanii na kuwasimamia haki zao mpaka wasajiliwe na BARAZA. Inamaanisha masaloon na maduka yanayotoa huduma za urembo na mavazi kwa wasanii wasifanye biashara yao mpaka wasajiliwe na BARAZA. Walinzi wa wasanii wasajiliwe na BARAZA. Inamaanisha taasisi zinazotetea haki za wasanii lazima wasajiliwe BARAZA ili wafanye kazi yao. Kanuni hii inaendelea na utaratibu wa kuvunja na kutokuheshimu haki za binadamu (Haki ya kushiriki kwenye shughuli za kitamaduni).

Ibara ya **(15)**, ibara ndogo ya **(3)** ya **Mkataba wa kimataifa wa haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni (1966)** inaelekeza kuwa *nchi mwanachama imejidhatiti kuheshimu* ***uhuru muhimu*** *kwa utafiti wa kisayansi na shughuli za ubunifu*. Kifungu hicho cha rasimu ya kanuni kinavunja mkataba huu wa kimataifa kwa kudhoofisha uhuru muhimu wa shughuli za kibunifu

Usajili huu umeweka nguvu kubwa kwenye kukusanya mapato kupitia ada bila kuzingatia misingi ya haki za binadamu.

Ikumbukwe usajili unaweza ukafutwa. Inamaanisha mtu akifutiwa usajili au asiposajiliwa haruhusiwi kutoa maoni yake kuhusiana na kazi za Sanaa, mfumo mzima wa uendeshwaji wa sekta ya sanaa au kushiriki katika kukuza Sanaa nchini. Hii ni kinyume na katiba ya nchi: -

Rejea ibara ya **18,** ibara ndogo **(1) na (2)** ya **katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)** kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara (Toleo la Kiswahili la mwaka 2000) inaelekeza *kila mtu ana uhuru wa kutoa maoni.*

Rejea ibara ya **21,** ibara ndogo **(2)** ya **katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)** kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara (Toleo la Kiswahili la mwaka 2000)

inaelekeza kuwa:

> *"Kila raia anayo haki na uhuru wa kushiriki kikamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye, Maisha yake au juu ya mambo yanayolihusu taifa"*

Kwa vifungu hivyo vya kanuni pendekezwa msanii hatoweza kushiriki kikamilifu kufikia maamuzi kwenye sekta ya Sanaa na utamaduni mpaka awe amesajiliwa. Vifungu hivyo vinaweka masharti juu ya uhuru wa wananchi kushiriki kikamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayowahusu, kitu ambacho ni kinyume na katiba ya nchi.

**Mapendekezo:** Kifungu hiki kinavunja haki za binadamu zinazolindwa na katiba ya nchi. Kinakinzana na malengo makuu ya uundwaji wa baraza. Kinaongeza utitiri wa usajili na kudhoofisha biashara ya Sanaa nchini. Azaki zinazojihusisha na haki za binadamu kwenye sekta ya Sanaa na utamaduni, tunatafsiri hiki kifungu kama tishio la kutudhoofisha katika jitihada za kulinda haki za binadamu kwa wasanii. Ni wajibu wa kikatiba kwa kila mtu kulinda haki za binadamu. Kifungu hiki ni tishio la msingi kwa wananchi kufurahia uhuru wao wa kutoa maoni kwenye sekta ya Sanaa na utamaduni. **Tafakuri: Itakuwaje kila sekta ili ushiriki lazima uwe umesajiliwa? Usajiliwe na Brela ili utoe maoni kuhusu biashara, usajiliwe na TCRA ili uweze kuangalia TV na kusikiliza taarifa ya habari, Usajiliwe na POLISI ili uweze kushiriki kwenye masuala ya usalama wa jamii, usajiliwe na wizara ya afya ili uweze kwenda hospitali, Usajiliwe na NEMC ili uweze kutunza mazingira?**

TARO
TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION

## 8 Kuzuia kusajiliwa kwa chama cha Sanaa chenye malengo sawa na chama kilichokwisha sajiliwa ni kuzuia ushindani wa vyama unaosababisha maendeleo ya Sanaa na pia ni kuminya haki ya kikatiba ya uhuru wa kushirikiana na wengine.

Kifungu cha **20**, kifungu kidogo **(2)(e**) cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinakataza usajili wa chama kuingilia shughuli za chama kingine ambacho hakijafutwa kwa mujibu wa Sheria.

Hii inaondoa ushindani baina ya vyama na inasababisha kudorora kwa sanaa nchini. Ikiwa itaruhusiwa chama zaidi ya kimoja kusajiliwa kufanya kazi moja, wanachama watachagua chama chenye viongozi wenye utendaji mzuri kwa maslahi yao. Hivyo basi wasanii watapata vyama bora kwasababu vyama vyote dhaifu vitakimbiwa na wanachama wake. Hii itaboresha shughuli za sanaa nchini kiasi cha kwamba hata mashirkisho yatakuwa imara. Kwasasa vyama vya Sanaa vimedhoofika kwasababu ya kuwa na uongozi mbovu na wasanii hawana namna ya kuvikimbia vyama hivyo kwasababu hakuna mbadala wake.

Rejea ibara ya **20,** ibara ndogo **(1)** ya **katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)** kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara (Toleo la Kiswahili la mwaka 2000) inaelekeza kuwa:-

> *"Kila mtu anastahili kuwa huru, bila ya kuathiri sheria za nchi, kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani kuchanganyika na kushirikiana na watu wengine, kutoa mawazo hadharani, na hasa zaidi kuanzisha au kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo."*

> Kuwa na vyama vya Sanaa Zaidi ya kimoja vinavyofanya kazi inayofanana hakuathiri sheria yoyote ya nchi. Kutengenezwa kwa kanuni hii kuna mzuia msanii kufurahia haki yake aliyopewa na katiba ya kuanzisha au kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo.

TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION

**Mapendekezo**: Kifungu hiki kinapaswa kurekebishwa na kuruhusu kusajiliwa kwa vyama vyenye malengo yanayofanana ili kuweka ushindani katika utoaji wa huduma wa vyama mbele ya wanachama wao ambao ni wasanii.

# 9 Mashirikisho yanapaswa kuzingatia misingi ya demokrasia inayompa kila msanii haki ya kushiriki kufanya maamuzi yanayoiathiri Sanaa yake.

Mfumo uliozoeleka wa kuendesha mashirikisho umepitwa na wakati na hauendani na misingi ya kidemokrasia ya nchi inayolindwa na katiba. Mfumo wa mashirikisho ya Sanaa kuundwa na vyama vya Sanaa uko sawa. Ila mfumo wa wawakilishi wachache kwenye vyama vya Sanaa pekee, kuwa na haki ya kufanya maamuzi kwenye mashirikisho hauko sawa, unahitaji marekebisho. Mfumo huo unawanyima wanachama wa vyama vya Sanaa haki ya kushiriki katika kufanya maamuzi yanayoathiri Sanaa yao. Rejea ibara ya **21,** ibara ndogo **ya (2)** ya **katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)** kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara (Toleo la Kiswahili la mwaka 2000) inaelekeza: -

> *"Kila raia anayo haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye, Maisha yake au yanayolihusu Taifa"*

**Mapendekezo:** Viongozi wa vyama vya Sanaa hawapaswi kuwa viongozi wa mashirkisho kwasababu tayari wanamajukumu mengine. Watumishi wa umma hawapaswi kuwa viongozi wa vyama vya Sanaa au mashirikisho kwa dhumuni la kuepusha mgongano wa kimaslahi.

Hivyo basi kunapaswa kuundwa "***Tume Huru ya Uchaguzi wa Mashirikisho ya Sanaa Nchini"*** itakayo kuwa na jukumu la kusimamia uchaguzi kwenye mashirikisho yote ya Sanaa nchini.

Tume iundwe na makatibu wa vyama vyote vya Sanaa vya kitaifa nchini, mwakilishi mmoja kutoka kila asasi ya maendeleo ya sanaa kwa ngazi ya kitaifa nchini, mwakilishi mmoja kutoka kila chama cha waandishi wa habari ngazi ya kitaifa nchini, mwakilishi mmoja kutoka kila chuo kinachotoa elimu ya Sanaa na utamaduni nchini. Ili kulinda uhuru katika uendeshwaji wa tume, watumishi wa umma hawapaswi kuwa sehemu ya uongozi wa tume bali wawe wanachama tu.

Kisha tume kuendesha uchaguzi wake wa kutafuta viongozi wa tume yaani ***Mwenyekiti, Katibu, Muwekahazina na Wajumbe wanne***. Jumla ya viongozi saba wataunda bodi ya tume kusimamia uchaguzi wa mashirikisho yote ya Sanaa nchini. Wanachama wote wa vyama vya Sanaa nchini wapewe haki ya kupiga kura na kupigiwa kura katika kuchagua viongozi wa mashirikisho. Uongozi ndani ya mashirikisho usizidi miaka miwili kwa awamu moja. Kiongozi asiruhusiwe kuongoza Zaidi ya awamu mbili. Kuendesha mashirikisho kwa kutokufuata uwazi, mfumo wa demokrasia na utawala wa sheria viwe sababu ya kumzuia kiongozi kugombea mara ya pili. Vigezo vya elimu na uzoefu katika uendeshaji wa taasisi vitumike kama vigezo muhimu kugombea nafasi za uongozi kwenye mashirikisho. Hii itasaidia maendeleo ya Sanaa nchini kwani mashirikisho yatakuwa hai yenye uwajibikaji.

**a) Mamlaka ya BARAZA kuharibu kazi ya Sanaa iliyo kinyume na sheria haijazingatia haki na maslahi ya msanii**

Kifungu cha **24,** kifungu ndogo cha **(2)** cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinaelekeza: -*"Pale ambapo Baraza litabaini kuwa kuna kazi za sanaa zilizotengenezwa au zinatengenezwa zimekiuka au zina mwelekeo wa kukiuka masharti ya Sheria, Kanuni hizi au Sheria nyinginezo za nchi, Baraza linaweza kuziharibu kazi hizo, au kutoa maelekezo mengine kwa kadiri itakavyoonekana inafaa."*

Kifungu hicho kinatoa nafasi ya baraza kufanya tafasiri potofu juu ya kazi za sanaa, kisha kufanya maamuzi yasiyozingatia misingi ya utoaji haki.

**Mapendekezo**: Kifungu hicho kifutwe na baraza lisipewe mamlaka ya kutathmini maana ya kazi ya sanaa nchini. Ili kazi ya sanaa iwafikie walaji/walengwa lazima ipitie vyombo vya mawasiliano. Kazi ya kudhibiti maudhui kwenye kazi za sanaa iachwe chini ya mamlaka zinazohusika na vyombo vya mawasiliano.

**b) Kumfutia usajili wa Baraza msanii au mdau ni kumvunjia haki zake za msingi za binadamu**

Kifungu cha **28,** kifungu kidogo cha **(1), (b),(c),(e)** cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinaelekeza kuwa sababu za kufutiwa usajili wa Baraza ni utendaji wa makosa ya jinai kwa mdau wa sanaa, kukiuka maadili ya kanuni au sababu baraza litakavyoona inafaa .

Ikumbukwe kanuni zimeweka wazi kuwa ni kosa kufanya sanaa bila usajili. Hivyo basi ukifutiwa usajili hutaruhusiwa kufanya tena kazi za sanaa. Ufanyaji shughuli za sanaa ni sehemu ya haki za binadamu (haki ya kufanya kazi na haki ya kitamaduni). Sheria haiwezi kutungwa kumuondolewa mwananchi haki zake za asili.

Hivyo basi kumfutia mdau usajili wa Baraza ni kumzuia mdau wa sanaa kufurahia haki zake za msingi za binadamu (Haki ya kufanya kazi na haki ya kushiriki kwenye shughuli za kitamaduni). Sanaa ni kazi inayompa kipato msanii kujikimu. Katiba ya nchi imempa kila mwananchi haki ya kufanya kazi ambayo haiwezi kupokwa na sheria yoyote. Baraza linaweza kumsajili msanii lakini haliwezi kumfutia usajili.

Rejea ibara ya **22,** ibara ndogo **(1)** ya **katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)** kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara (Toleo la Kiswahili la mwaka 2000) inaelekeza: - *"Kila mtu anayo haki ya kufanya kazi"*

Kwa mujibu wa **Sheria ya Sanaa 1984, na marekebisho yake ya sheria namba 5 ya 2019**, Baraza halina mamlaka ya kushughulikia masuala yaliyo nje ya Sanaa na utamaduni. Masuala yanayohusiana na makosa ya jinai kwa msanii yanasimamiwa na sheria za makosa ya jinai na mamlaka husika.

Maisha binafsi ya msanii sio jukumu la Baraza. Baraza linahusika pale tu Sanaa inapohusika. Msanii akifanya makosa ya jinai kwenye Maisha yake ya kawaida, hio haihusiani na Sanaa.

**Mapendekezo:** Kifungu hicho cha kanuni kinakandamiza misingi ya haki na hakina mantiki yoyote zaidi ya unyanyasaji na kuongeza udhibiti wa wasanii na kuhodhi maisha binafsi ya wasanii. Sheria za nchi hazitaki mtu aliyekutwa na makosa ya jinai kuendesha taasisi za umma na sio shughuli zake binafsi.

Hivyo basi kifungu cha kufutiwa usajili na sababu zake za kufutiwa usajili vitumike kwa taasisi pekee na sio msaniii (mtu binafsi). Pia usajili wa wadau wa Sanaa ufanyike kwa lengo la kujenga kanzi data ya sekta na sio kudhibiti wasanii au wadau. Usajili usitumike kumzuia mdau kufanya shughuli yoyote ya Sanaa nchini. Kuwa na vifungu vya namna hiyo kwenye sekta ya Sanaa na utamaduni ni kuweka haki za msingi za wasanii rehani.

# 11 Kuweka kibali ili msanii aweze kufanya kazi ya Sanaa ni kuminya haki za binadamu (Haki za kitamaduni)

Kifungu cha **3** na Kifungu cha **15,** kifungu kidogo cha **(1)** na **(2)** cha **rasimu ya kanuni pendekezwa** vimeweka kibali kwa msanii ili aweze kufanya kazi za Sanaa nchini.

Ikumbukwe sanaa ni haki ya binadamu ya kufanyakazi na haki ya kitamaduni. Sanaa ni tamaduni ya mtanzania. Ikifikia hatua jamii haiwezi kufurahia tamaduni zake mpaka iombe kibali hiyo inaashiria wazi Baraza limekiuka malengo ya uundwaji wake yaliyopewa na sheria kwa kudhoofisha tamaduni nchini**.**

Rejea kifungu cha **35** cha rasimu ya kanuni pendekezwa chenye maudhui yanayolandana na kifungu cha hapo juu.

Tanzania ni nchi mwanachama na imesaini mikataba ya kimataifa ya kulinda na kuheshimu haki za binadamu (haki za kitamaduni) tangu **1966**.

Rejea **Mkataba wa kimataifa wa haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni (1966)** kupitia ibara ya **(15)**, ibara ndogo ya **(1) (a)** inaelekeza kuwa *nchi mwanachama inatambua haki ya kila mtu kushiriki kwenye maisha ya kitamaduni*.

Ambapo ibara ya **(15)**, ibara ndogo ya **(3)** ya mkataba huo tajwa hapo juu unaelekeza kuwa *nchi mwanachama imejidhatiti kuheshimu uhuru muhimu kwa utafiti wa kisayansi na shughuli za ubunifu.*

Sanaa ni moja ya shughuli za kibunifu zinazohitaji uhuru wake muhimu kuheshimiwa.

Ikumbukwe kufutwa kwa ***Sheria ya Baraza la Sanaa la Taifa (1974)*** *na* ***Sheria ya Baraza la Muziki la Taifa (1974),*** kisha kutungwa ***Sheria ya Sanaa ya Taifa, namba 23 ya (1984)*** ni jitihada za serikali kulinda haki za binadamu za kitamaduni ili kuendana na mikataba ya kimataifa. Kabla ya mwaka **1984**, sheria hizo zilikua hazitambui masuala ya kitamaduni.

Tanzania ilianza kutambua haki za binadamu rasmi mwaka **1984** ndipo katiba ya nchi ilipofanyiwa marekebisho. Ambapo mwaka huo ndipo mamlaka moja ya sanaa (Baraza la sanaa la Taifa) iliundwa nchini ili kuanza utekelezaji wa kutambua na kulinda haki za kitamaduni rasmi.

Hivyo basi Tanzania ilichukua **miaka nane** (1976-1984) toka kutambua haki za kitamaduni mpaka kuanza kuzitekeleza. Kwahiyo kuweka kibali kama sharti la kufurahia haki ya binadamu inayolindwa kimataifa ni kuvunja haki hiyo. Sanaa ni utamaduni. Haiwezekani mtanzania asifurahie utamaduni wake mpaka awe na kibali cha baraza.

Ikumbukwe utamaduni wa mtanzania ulikuwepo kabla ya baraza kuundwa. Baraza halikuundwa kudhoofisha utamaduni bali kuhamasisha, kudumisha na kukuza utamaduni. Kifungu tajwa cha kanuni kinadhoofisha na kudumaza utamaduni wa mtanzania kwa kuchochea wananchi kuacha kushiriki kwenye shughuli za kitamaduni kutokana na masharti magumu na gharama kubwa.

Haiwezekani mtanzania asicheze ngoma zake za asili mpaka awe na kibali, haiwezekani wanakijiji wasiwasimulie hadithi watoto wao mpaka wawe na kibali, haiwezekani wakina mama Iringa wasishone vikapu (vitangula) mpaka wawe na kibali, haiwezekani watanzania wasiabudu kwa nyimbo, maigizo na sala zitungwazo mpaka wawe na kibali, haiwezekani wanawake wasichorwe hina mpaka wawe na kibali, haiwezekani, kijijini wasifinyange vyungu vya kupikia mpaka wawe na kibali, haiwezekani wasanii wachanga wasijifunze Sanaa kivitendo kwa kukusanyika na kufanya mazoezi ya kufanya matamasha , uandishi mpaka wawe na kibali, Haiwezekani msanii asifanye ujasilia mali wa kuchora mabango madogo madogo mitaani mpaka awe na kibali. Haiwezekani shughuli za kijasiliamali kama watengeneza shanga wasifanye na kuwauzia watalii mpaka wawe na kibali. Hiki kibali ni urasimu, ukandamizaji na udhoofishaji wa Sanaa, uchumi na uvunjifu wa haki za binadamu za utamaduni.

Baraza liwe na ubunifu na litafute njia nyingine halali yenye mantiki ya kujiingizia mapato sio kibali. **Kibali kwenye Sanaa kwa wasanii ni ukiukwaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa moja ya malengo makuu ya uundwaji wa baraza.**

**Mapendekezo:** Msanii kutokusajiliwa baraza isiwe kosa, ni jukumu la baraza kufanya kazi ya kukuza Sanaa na utamaduni nchini kiasi cha kwamba wasanii na wadau waone kuna umuhimu wa wao kujisajili kwa hiari yao. Kujisajili baraza kuwe kama kujisajili COSOTA, sio lazima bali ni utambuzi wa msanii ili aweze kulinda haki zake kiurahisi. Msanii apate hasara ya kutokujisajili baraza kwa kukosa kushiriki katika fursa mbailimbali zinazopitia au zinazohitaji utambuzi wa baraza. Kujisajili kwa msanii isiwe lazima wala kutokusajili kusiwe kosa.

Kifungu cha **29,** kifungu kidogo cha **(3)** na **(4)** cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinampa Katibu, afisa yeyote wa Baraza au mtu yeyote anayetekeleza majukumu ya Baraza kuingia katika majengo yanayofanyiwa kazi za Sanaa na kukagua bila ruhusa ya wahusika au ruhusa ya mahakama.

Kifungu hicho tajwa cha kanuni kimetoa mamlaka makubwa kuliko polisi wanaolinda usalama wa wananchi na mali zao.

Mtu yoyote haruhusiwi kumzuia Katibu, afisa yeyote wa Baraza au mtu yeyote anayetekeleza majukumu ya Baraza kuingia katika jengo kwa kigezo kuwa anamzuia afisa huyo kufanya kazi yake. Hii ni kinyume na sheria zetu zinazoongoza makosa ya jinai **(sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai, sura ya 20 mapitio ya mwaka 2019)**, pia ni kinyume na haki za binadamu zinazolindwa na katiba **(Haki ya faragha).** Hata polisi wakitaka kuingia kupekua kwenye jengo la mtu lazima wapewe kibali cha mahakama au kama ni dharura kwa madhumuni ya kulinda usalama wa wananchi kuna utaratibu wa kufuata ambao unahusisha kushirikishwa kwa viongozi wa serikali ya mtaa au Kijiji, na kama kupekua kunahusisha nyumba yenye mwali, basi polisi wanapaswa kumpa nafasi mwali kuondoka katika jengo ili wapekue.

Tunaelewa miundo mbinu ya Sanaa inahusisha kumbi, majengo ya starehe na makazi ya watu binafasi. Kuruhusu kuwa na kifungu kama hicho ni kuhalalisha maafisa wa baraza kuvunja haki ya binadamu ya faragha bila kuhojiwa. Hii ni kinyume na uundwaji wa baraza. Kanuni hii pia inaruhusu Afisa wa baraza kuingia kwenye nyumba ya mtu binafsi bila ruhusa ya mahakama akaanza kukagua na kuingilia shughuli zinazofanyika. Kifungu hicho kinavunja haki za binadamu (haki ya faragha), kinatengeneza hofu na woga kwa wadau wa Sanaa na jamii kwa ujumla dhidi ya baraza. Kinamfanya afisa wa baraza aweze kuingilia shughuli za Sanaa popote pale kwa muda wowote ule na kuamrisha shughuli isimame. Kifungu hiki kinamwezeshesha afisa wa baraza kuwa na nguvu ya kulazimisha rushwa kwa wasanii na wamiliki wa miundo mbinu.

Kifungu hiki kinaendeleza mwenendo wa baraza kubadilisha muelekeo wa lengo kuu la uundwaji wa baraza. Baraza halikuundwa kudhibiti wasanii bali kusaidia wasanii. Kuna sheria na mamlaka za kutosha zinazodhibiti kazi za Sanaa na wasanii. Sio sahihi baraza kujiongezea mamlaka yaliyo nje ya kusudio la uundwaji wake.

**Mapendekezo:** Baraza linapswa kushirikiana na mamlaka nyingine za serikali zilizopewa dhamana ili kutekeleza majukumu yake. Baraza sio Kisiwa ni taasisi ya serikali na inapaswa kufanya kazi kwa kuzingatia misingi ya utawala bora hususani mgawanyo wa majukumu na taasisi nyingine za serikali, sio kujiwekeza katika kujilimbikizia mamlaka ifanye kila kitu yenyewe isishirikiane na mamlaka nyingine.

**Baraza kuingilia uhuru wa asasi za kiraia katika utekelezwaji wa majukumu yake**

Kifungu cha **30,** kifungu kidogo cha **(1)** na **(2)** cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinaelekeza kuwa Baraza litapitia maandiko ya miradi ya Sanaa kabla ya kutekelezwa.

Sheria ya Asasi zisizo za kiserikali **(Non-Governmental Organization Act. 2002)** imetoa uhuru wa Azaki kufanya kazi bila kuingiliwa na serikali. Azaki ni taasisi huru zinazotekeleza majukumu yake kutokana na mahitaji ya jamii inavyoona.

Pia **sheria ya Asasi zisizo za kiserikali (2002),** imempa mamlaka msajili wa AZAKI kupokea taarifa zote muhimu kuhusu utekelezwaji wa miradi wa AZAKI nchini.

Baraza kuandika vifungu vilivyoorodheshwa hapo juu ni kuingilia sheria nyingine za nchi na mamlaka za taasisi nyingine za serikali. Pia ni kudhoofisha uhuru wa azaki katika utendaji wake. Hili linaweza kutafsiriwa kama jitihada za kujilimbikizia mamlaka kwa ajili ya kupata nguvu ya kudhibiti wadau wote wa sanaa ambalo sio lengo la uwepo wa baraza. Sekta haiwezi kusaidiwa kwa kudhibitiwa bali kuwezeshwa.

Tangu 2018 baraza limepoteza muelekeo na kuanza kujikita katika kufanya marekebisho ya sheria kwa lengo la kujilimbikizia mamlaka kwenye kazi ambazo tayari sheria zingine za nchi zimekwisha weka wazi taasisi zinazohusika. Madhara yake inatengeneza mgongano wa kimaslahi baina ya taasisi za serikali.

Haiwezekani Baraza lipitie maandiko ya miradi wakati halina uwezo wa kuwezesha miradi, halina wataalamu wa kutosha kwenye masuala ya miradi inayogusa sekta mbalimbali. Miradi huandikwa kwa matwakwa ya muwezeshaji na sio vinginevyo. Miradi ikishapitishwa na wahisani haiwezi kubadilishwa, hivyo basi baraza kuingilia utekelezaji wa shughuli za Azaki ni kuvunja uhuru wa azaki unaolindwa na sheria za ndani za nchi, maazimio ya Umoja wa Mataifa na mikataba ya kimataifa inayolinda haki za binadamu.

Haiwezekani kupeleka miradi ya kutetea haki za binadamu ikakaguliwe na taasisi ambayo inaweza kulalamikiwa kwa uvunjifu wa haki za binadamu, huko ni kutengeneza mgongano wa kimaslahi na AZAKI. Hii kwa upande wa AZAKI inaweza tafsiriwa ni moja ya jitihada za kutudhoofisha au kutunyamazisha ili tusiweze kushughulikia masuala yanayoathiri haki za binadamu za wasanii. Haki za binadamu ni stahili ya kila binadamu.

**Mapendekezo:** Kifungu hicho kifutwe kwani kinalenga kukandamiza uhuru wa kufanya kazi wa AZAKI zinazoshughulikia masuala ya haki za binadamu kwenye sekta ya Sanaa, kinapaswa kupigwa vita na kufutwa kwani hakiheshimu misingi mikuu ya demokrasia, utawala wa sheria, utawala bora na haki za binadamu.

# 14 Vibali kwa wasanii wadau wa Sanaa au kikundi cha Sanaa kwenda nje ya nchi kufanya sanaa ni kuvunja haki za binadamu za kitamaduni na kuingilia kazi za mamlaka nyingine za nchi.

Kifungu cha **31** cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinaelekeza kuwa wasanii, wadau wa Sanaa au kikundi cha Sanaa kinapaswa kuwa na kibali ili kwenda nje ya nchi kufanya kazi za Sanaa. Kifungu hicho kinaelekeza dhumuni lake ni kushughulikia masuala ya kidiplomasia kwa wasanii, wadau au kikundi wakiwa nje ya nchi.

Kifungu hiki hakina mantiki yoyote ile zaidi ya kuendeleza lengo lisiliofaa la baraza kujilimbikizia mamlaka ili kukandamiza uhuru muhimu wa kufanya shughuli za ubunifu.

Rejea **Mkataba wa kimataifa wa haki za kiuchumi, kijamii na kitamaduni (1966)** kupitia ibara ya **(15)**, ibara ndogo ya **(3)** unaelekeza kuwa *nchi mwanachama imejidhatiti kuheshimu uhuru muhimu kwa utafiti wa kisayansi na shughuli za ubunifu*. Sanaa ni moja ya shughuli za kibunifu zinazohitaji uhuru wake muhimu kuheshimiwa na kulindwa.

Baraza kutengeneza kifungu hiki cha kanuni ni kuingilia majukumu ya mamlaka nyingine. Sheria imeunda wizara ya mambo ya nje, Jeshi la polisi, ofisi ya mwanasheria mkuu wa serikali, Ofisi ya mwendesha mashtaka na Mamlaka ya uhamiaji kushughulikia masuala yote ya wananchi kwenda na wawapo nje ya nchi.

**Mapendekezo:** Kifungu tajwa kinapaswa kufutwa na kutupiliwa mbali hakina faida kwa wasanii, hakiendani na malengo ya uundwaji wa baraza. Kinavunja haki za binadamu za kitamaduni za uhuru wa wasanii kufanya kazi za Sanaa, kinaleta urasimu kwenye shughuli za sanaa na kinaingilia mamlaka nyingine za serikali. Msanii anapewa mzigo mzito katika kuendana na sheria, anakuwa anajukumu la kurudia mambo yale yale kwa mamlaka zaidi ya moja.

# 15 Vibali vya kuingia nchini kufanya kazi za Sanaa ni urasimu usio na tija na kuingilia kazi za mamlaka nyingine za nchi.

Kifungu cha **32** cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinaelekeza kuwa Msanii au kikundi chochote cha sanaa kutoka nje ya Tanzania kinaweza kufanya tukio la Sanaa hapa nchini baada ya kupata kibali kutoka Baraza.

Kifungu hiki ni moja ya vifungu vinavyoingilia kazi za mamlaka nyingine za serikali. Mamlaka ya uhamiaji wamepewa jukumu na sheria kutoa vibali vya kufanya kazi nchini ikiwa mhusika ni raia wa kigeni. Baraza kuweka kifungu cha kibali ni muendelezo wa kujilimbikizia mamlaka za taasisi nyingine za serikali kwa ajili ya udhibiti wa sanaa ambao sio lengo la uundwaji wake. Baraza liliundwa kwa lengo la kusaidia ukuaji wa sekta na sio kudhibiti sekta. Mwaka 2018 baraza lilianza kubadilisha mwelekeo wa utendaji wake na kujikita katika kudhibiti sekta.

Ikumbukwe mwekezaji anaweza kuacha kuwekeza kwenye sanaa nchini kutokana na utiriri wa vibali visivyo na tija. Mfano: -

i. Mwekezaji ana ukumbi- atalipa kibali cha miundo mbinu ya sanaa

ii. Kama ukumbi unaonyesha filamu-Kibali cha kuonyesha filamu

iii. Mwekezaji anaendesha matamasha- Kibali cha kujihusisha na sanaa

iv. Mwekezaji analeta msanii kutoka nje- Kibali cha msanii kutoka nje

v. Mwekezaji ataandaa tamasha- Atalipa kibali cha kuendesha tamasha

vi. Mwekezaji atalipa gharama zote za msanii

vii. Mwekezaji atalipa kodi ya TRA

viii. Mwekezaji atalipia mirabaha ya kazi za muziki na filamu

ix. Mwekezaji atalipia leseni ya kutumia kazi zinazolindwa na hakimiliki

x. Mwekezaji atalipa vibali vya kufanya kazi na kukaa nchini

Kutokana na urasimu ulioletwa na sheria wawekezaji wengi kwenye sekta ya sanaa wanajikita kuwekeza Kenya na Afrika ya kusini. Ikumbukwe hapo bado vibali kutoka bodi ya filamu ikiwa muwekezaji atajihusisha na sanaa ya filamu. Pia kifungu hiki kinachochea kupunguza ukuaji wa sanaa kimataifa kwasababu ya gharama kubwa na urasimu kwa wasanii wa kigeni kuja nchini.

**Mapendekezo:** Kifungu hiki kifutwe ili kuondoa urasimu na gharama zisizokuwa za lazima ili kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji pia kuheshimu haki za binadamu

## 16 Uthibitisho wa uwezo wa kumudu gharama kwa muandaaji wa kigeni ni urasimu usio na mantiki, pia ni kuingilia utendaji wa mamlaka ya uhamiaji

Kifungu cha **33** cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinaelekeza kuwa mgeni hawezi kufanya tukio la Sanaa mpaka muandaaji athibitishe uwezo wa kumudu gharama za undeshwaji wa tukio.

Inatokea mara nyingi msanii kutoka nchi moja kuomba kushiriki katika tamasha la nchi nyingine bure bila kulipwa ili kujitambulisha katika soko la Sanaa la nchi ile. Hivyo basi kanuni hii itawazuia waandaji wetu kuwaruhusu wasanii wa kigeni kuja nchini kujitolea. Kujitolea kunasaidia ukuaji wa sekta kwa muunganiko na wasanii wa nchi nyingine. Nchi zenye mafanikio makubwa ya sanaa duniani hazina masharti hayo magumu kwenye sekta ya sanaa bali yapo kwenye utaratibu wa mgeni yoyote kuingia kwenye nchi.

Pia kuna wakati wasanii wetu huwakaribisha wasanii wa kigeni nchini, lakini kwa makubaliano wataishi kifamilia kipindi wapo nchini ili kupunguza gharama za maisha. Pia hata hii inafanyika kwa wasanii wetu wakienda nje ya nchi. Hivyo basi kuwa na kanuni hii kunavuruga utaratibu wa kufurahia fursa za kibiashara kwa gharama za chini.

Faida yake kama msanii wa kigeni ambaye ni maarufu atakuja nchini kwa utaratibu wa hapo juu, basi atalitambulisha jukwaa la nchi kimataifa, pia wasanii wa nchini watapata nafasi ya kushirikiana na msanii yule ili kuweza kulitumia soko la alipotoka. Tukiweka masharti magumu wasanii wa nje hawatakuja Tanzania. Wataenda nchi za jiirani na sanaa yetu itadorora.

**Mapendekezo:** Kifungu hicho kifutwe chote hakina faida kwa sanaa wala msanii bali kinaongeza udhibiti kwa wasanii usio na tija.

TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION

a) **Uandaaji wa matukio ya Sanaa ni biashara usiingiliwe na baraza.**

Kifungu cha **34** cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinaelekeza kuwa mwandaaji aliyeleta msanii au kikundi cha sanaa kutoka nje ya nchi anao wajibu wa kuakikisha tukio linafanyika kama lilivyopangwa. Hii kanuni haiendani na mazingira ya kibiashara katika sekta ya Sanaa. Kuna wakati uendeshwaji wa matukio unatokea kuwa na ulazima wa kubadilika ili kumnusuru mwandaaji kwenye mazingira ya kupata hasara, mfano kubadilisha eneo la kufanyia tukio, siku ya tukio, ratiba na namna nzima ya uendeshaji kutokana na sababu mbalimbli zilizo nje ya uwezo wa mwandaaji. Kifungu hiki kimezungumzia suala pana kwa ufinyu wa hali ya juu. Inafaa kuheshimu uwepo wa sheria nyingine za nchi zilizoandaliwa kushughulikia masuala ya namna hiyo hususani sheria ya mikataba, sura ya 345 mapitio ya 2002. Masuala ya kibiashara ni masuala ya kimikataba, yaachwe yaongozwe na sheria za mikataba.

**Mapendekezo:** Kifungu hicho kifutwe chote hakina mantiki kwa sanaa wala msanii bali kinaongeza udhibiti kwa wasanii usio na tija na kutengeneza mazingira ya baraza kuingia kwenye migogoro na wadau. Ni jukumu la msanii wa kigeni kujihakikishia mazingira mazuri ya kibiashara kabla ya kuja kufanya tamasha nchini.

b) **Suala la kutambua mambo ya kimaadili ya jamii ni jambo pana lililo nje ya uwezo wa baraza pekee, baraza kuandaa kanuni hizi bila kushirikisha wadau mbalimbali wa masuala ya kijamii kunapelekea maadili kujadilika kiufinyu.**

Kifungu cha **37** na **38** cha rasimu ya kanuni pendekezwa kinaelekeza masuala ya kimaadili. Ikumbukwe masuala ya kimaadili ya jamii ni mambo ya kitaalamu yanayohusisha kada mbalimbali na makundi mbalimbali katika jamii. Hatujawahi kuona wala kusikia baraza likiitisha mikutano ya kitaifa kujadiliana kuhusu maadili ya Kitanzania ili kupata mapendekezo ya kisomi, kitaalamu, kiuzoefu na kimkakati. Tumeshuhudia kuona masuala ya kimaadili yakiamuliwa kimihemko na kimitazamo binafsi ya maafisa wa baraza bila kujali haki za binadamu na misingi ya utoaji haki. Hali hii ni hatari sana kwa sekta ya Sanaa. Mpaka sasa kazi kadhaa za sanaa zimefungiwa na kusababisha hasara kubwa kwa wawekezaji bila kuwa na mwongozo unaeleweka na kukubalika katika jamii. Hii inasababisha kuwepo kwa fikra na hisia za ukandamizaji na upendeleo baina ya wasanii. Kuna kazi za ndani zinafungiwa huku kazi za nje zilizo na sifa sawa zikiendelea kuonyeshwa mpaka hivi sasa kwenye vyombo vya habari.

**Mapendekezo**: Masuala yote ya maadili yanapaswa kuwa na kanuni zake zinazojitegemea. Kwa mantiki hiyo; inashauriwa kuandaa rasilimali ili kuwekeza kwenye kushirikisha na kuruhusu ushiriki wa wadau mbalimbali wa masuala ya kimaaadili nchini kutoa maoni ili kutengeneza kanuni iliyo ya haki na yenye tija inayoheshimu haki za binadamu. Vifungu hivyo tajwa tunapendekeza vifutwe.

a) **Kazi za Sanaa katika vyombo vya habari sio jukumu la baraza bali ni la mamlaka ya mawasiliano**

Kifungu cha **39** na **40** ya rasimu ya kanuni pendekezwa vinaongelea masula ya uzingatiaji wa maadili ya kazi za Sanaa kwenye vyombo vya habari.

Vifungu hivyo vinaendeleza jitihata za baraza kujilimbikizia mamlaka na kungilia majukumu ya mamlaka nyingine za serikali ili kudhibiti sanaa. Ni jukumu la kisheria kwa Mamlaka ya mawasiliano (TCRA) kushughulikia masuala yote ya maudhui katika vyombo vya habari. Tayari sheria na kanuni zipo zinazosimamia masuala ya maadili kwenye maudhui ya vyombo vya habari. Baraza halipaswi kuingilia utendaji wa TCRA. Baraza linapaswa kutambua na kuheshimu misingi ya utawala bora ambayo inajumuisha mgawanyiko wa majukumu baina ya mamlaka za serikali.

**Mapendekezo:** Vifungu hivyo tajwa tunapendekeza vifutwe.

b) **Baraza halipaswi kujishughulisha na utatuzi wa migogoro**

Kifungu cha **41, 42, 43, 44** vya rasimu ya kanuni pendekezwa vinaipa baraza mamlaka ya kusuluhisha migogoro kwenye sekta ya sanaa. Hii ni nje ya dhumuni kuu la uundwaji wa baraza. Baraza halikuundwa kuwa chombo cha usuluhishi wala mahakama.

Hii inaleta mkanganyiko na mgongano wa kimasalahi na wasanii katika utendaji wa baraza. Hivyo basi baraza halipaswi kujihusisha na masuala ya migogoro ya wasanii kwasababu zifuatazo: -

a) Baraza linajishughulisha na kazi za Sanaa hivyo basi kuna uwezekano mkubwa kutokea mgogoro au mgongano wa maslahi kati ya baraza na msanii. Ikitokea hivyo malalamiko yatasilikilzwa wapi? Haiwezekani hakimu akawa hakimu wa kesi yake. Hivyo basi baraza halipaswi kuwa msuluhishi.

b) Baraza halina rasilimali kwa ajili ya kuendesha shughuli ya usuluhishi nchi nzima ambayo ni taaluma ya sheria. Usuluhishi ni taaaluma ya wanasheria, haiwezekani kuendesha sekta ya Sanaa kwa kutegemea hekima za watu wasio wanasheria. Pia kuna taasisi za haki nchini zenye rasimali, zinazoweza kuifanya kazi hiyo kwa ufasaha kabisa. Mfano. Tanzania International Arbitration commission **(TIAC)** na Tanganyika Law society **(TLS).** Ni vyema taasisi hizo zikatumika**.**

c) Pia migogoro ya wasanii inahusiana na mikataba, ambapo hilo ni eneo linalohitaji utaalamu wa sheria za mikataba. Sio suala la uzoefu wala mazoea. Baraza halina miundo mbinu na wataalamu. Pia kwa mujibu wa sheria, masuala ya mikataba yanaweza kuamuliwa na mahakama peke yake.

**Mapendekezo:** Ili kuondoa mgongano wa maslahi kati ya wizara na wasanii, wizara na baraza, wasanii na Baraza, vifungu hivyo vinapaswa kufutwa na mfumo mzima wa kutatua migogoro kwenye sekta ya Sanaa upelekwe kwenye wizara inayojihusisha na masuala ya haki nchini, kupitia taasisi zake kama Tanzania International Arbitration commission **(TIAC)**, Tanganyika Law society **(TLS)** na kadhalika.

# 19 Uandaaji wa kanuni pendekezwa haujazingatia usawa wa kijinsia

Kanuni zimekuwa kipofu wa kuzingatia mahitaji na mawazo ya jinsia zote kwa usawa. Hakuna kipengele chochote kinachohamasisha usawa wa kijinsia kwenye kuwezesha fursa sawa kwa wanawake na wanaume katika sekta ya Sanaa na utamaduni kuzifikia na kuzitumia rasilimali zilizopo. Uundwaji wa mashirikisho, kamati, mitandao na vyama vya Sanaa na utamaduni haujazingatia muundo wa uendeshaji unaotoa fursa sawa kwa wanawake katika ngazi za kutoa maamuzi.

**Mapendekezo:** Kanuni zinapaswa kuwa na vipengele vinavyowezesha jinsia zote kuwa na fursa sawa za kushiriki katika kufanya maamuzi kuanzia, kamati, mashirikisho, mitandao na vyama vya Sanaa na utamaduni

TARO
TANZANIA ARTISTS RIGHTS ORGANIZATION

# HITIMISHO

Tanzania Artists Rights Organization (TARO) imepitia rasimu ya Kanuni Pendekezwa kwa minajili ya kupitishwa na kutumika kwa shughuli za utendaji katika sekta ya Sanaa na utamaduni nchini; kwenye kanuni pendekezwa tumegundua masuala muhimu ambayo **yanaweza kutia doa taswira ya serikali** kwa sababu ambazo tumeshazielezea kwenye mapendekezo ya marekebisho.

TARO imeona kanuni pendekezwa zinashawishi mawazo na mtazamo unaotia shaka katika utekelezwaji wake ambao unaweza kuathiri ukuaji wa Sanaa na utamaduni kwa kiwango kikubwa. Haki za binadamu ambazo zimetambuliwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muunganmo wa Tanzania na mazingira ya biashara ya Sanaa nchini vimepuuzwa katika uandaaji wa kanuni hizi pendekezwa. Mtazamo wetu umegundua yafuatayo: -

a) Kanuni pendekezwa zimejikita kwenye kulipa baraza mamlaka ya kuwa mwamuzi wa hatima ya Sanaa nchini badala ya jukumu lake la msingi la kulea na kukuza Sanaa na utamaduni.
b) Katika vipengele vingi vya kanuni pendekezwa, hakuna vipengele vinavyoelekeza ukuaji na uendelezaji wa Sanaa. Vipengele vingi vimelipa baraza mamlaka ya kudhibiti kunufaika na haki ya msingi ya utamaduni.
c) Sheria ya Sanaa ya Taifa ambayo inasimamiwa na Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) imelekeza Baraza kulea, kukuza na kuendeleza Sanaa na utamaduni, lakini pia kupitia kanuni pendekezwa inaonesha Baraza linahofia uhuru na haki za wasanii kama tishio kwake na kuunda kanuni zinazokandamiza uhuru muhimu wa ubunifu unaolindwa na mikataba ya kimataifa ya haki za binadamu
d) Kanuni za Baraza la Sanaa la Taifa zilizopitishwa mwaka 2018, ambazo bado zinaendelea kutumika zimekua zikilalamikiwa na wadau wa Sanaa nchini kuvunja haki za binadamu, ikapelekea kuandikwa kwa Rasimu ya Kanuni pendekezwa; ambazo kwa kushangaza zimeonyesha kiwango kikubwa cha uvunjaji wa haki za binadamu zaidi ya kanuni zilizopo.

**ASANTE**

**“KAZI IENDELEE”**